BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA KUMI

Kikao cha Tano – Tarehe 21 Februari, 2023

Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua zitasomwa.

## I. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

**Mwenyekiti wa Kamati ya Ustawi wa Jamii:**

Hotuba ya kuwasilisha Ripoti ya Kamati ya Ustawi wa Jamii ya mwaka 2022/2023.

## II. MASWALI:

**Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:**

91. MHESHIMIWA SALHA MOHAMED MWINJUMA (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:

    Hivi karibuni kumeibuka na kushamiri vitendo vya kihalifu kama kukaba, kupiga na kupora mali za wananchi na wanaofanya vitendo hivyo wengi wao ni vijana wanaokadiriwa kuwa na umri wa miaka 10 hadi 25 ambao ndio nguvu kazi ya Taifa letu.

    (a) Je, ni ipi kauli ya Serikali katika kuwanusuru watoto na vijana wetu hao wanaojihusisha na vitendo hivyo.

    (b) Je, Serikali imejipanga vipi kuwanusuru wananchi wanaofanyiwa vitendo kama hivi.

**Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:**

22. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Pindi ukikamilika kwa wakati muafaka ujenzi wa Vituo vya Wajasiriamali vya Kifumbikai, Wete Pemba; Michakaini, Chake Chake Pemba, Kipitacho na Mkoani, Pemba vitakuwa ni alama na mfano mzuri wa juhudi za Serikali katika kuleta mageuzi ya kiuchumi na mpango madhubuti wa kuwaongezea kipato wananchi wa kawaida. Hata hivyo, kasi iliyoanza ya ujenzi huo imefifia na kutia mashaka kukamilika kwake kwa wakati.

(a) Je, ni kwa nini ujenzi wa vituo hivyo umezorota na kutia mashaka kukamilika kwake kwa wakati.

(b) Je, ni juhudi zipi za kifedha na za kiutawala za Serikali katika kuhakikisha kwamba vituo hivyo vinamaliza kujengwa na kuanza kutumika kwa wakati.

## Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

107. MHESHIMIWA KOMBO MWINYI SHEHE (Jimbo la Wingwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

Serikali kwa kiasi fulani imejielekeza kuwatatulia kero wananchi wake kwa kuwajengea miradi mbali mbali ikiwemo barabara, maji safi na salama, masoko, hospitali na mengi mengineyo.

(a) Je, kabla ya kutekelezwa kwa miradi hiyo, ni kwa kiasi gani Serikali inaishirikisha jamii husika kwa lengo hasa la kupatikana tija na ufanisi kupitia miradi hiyo.

(b) Je, ushirikishwaji wa jamii katika miradi hiyo huanzia hatua zipi.

## Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

24. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

Tasnia ya sanaa hususan ya maigizo imeendelea kukua kwa kasi kubwa na kuweza kutoa mchango mkubwa wa kuliingizia Taifa mapato.

(a) Je, Wizara yako ina mpango gani wa kuwasaidia wasanii hao kwa kuwapatia mikopo nafuu itakayowawezesha

kujiendesha wenyewe.

(b) Je, Wizara yako inautumia utaratibu upi wa kuwawezesha wasanii hao kujiendesha wenyewe.

**Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:**

31. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Pamoja na kukamilika kwa ujenzi wa Skuli ya Urafiki, miundombinu ya vyoo katika skuli hiyo haiko rafiki kwa suala zima la usafi na mazingira ya kujifunza na kufundishia skulini hapo.

Je, ni lini Wizara yako italiondoa tatizo hili ambalo limekuwa ni la muda mrefu sana.

33. MHESHIMIWA HABIB ALI MUHAMED (Jimbo la Mtambwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Serikali kupitia Wizara ya Elimu ilianzisha mfumo uliojulikana kama 'INFO SCHOOL' ambao ulilenga kurahisisha utunzaji wa kumbukumbu za wafanyakazi maskulini.

Je, faida zipi zilizopatikana maskulini kupitia mfumo huo.

**Wizara ya Afya:**

40. MHESHIMIWA ZAWADI AMOUR NASSOR (Jimbo la Konde) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Tunaipongeza Serikali kwa juhudi za kuboresha huduma za afya katika hospitali zetu. Pamoja na juhudi hizo, kuna baadhi ya vifaa vimekaa bila ya kutumika sambamba na taarifa ya kuwepo kwa mtambo wa "Ultrasound" katika kituo cha nyumba za maafa Tumbe.

(a) Je, kuna usahihi wa taarifa hiyo.

(b) Kwa kuwa kumekuwa na tatizo kubwa la huduma ya "Ultrasound" katika hospitali ya Micheweni, Je, Wizara ina mpango gani wa kuanzisha huduma hiyo katika hospitali hiyo.

(c) Je, ni muda gani tokea kuwepo mtambo wa "Ultrasound"

katika kituo hicho na ni sababu zipi zilizopelekea hadi sasa kushindwa kutoa huduma kwa akina mama.

<u>Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale:</u>

28. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale:

Kwa muda mrefu suala la muingiliano wa majukumu baina ya Idara ya Makumbusho na Mambo ya Kale pamoja na Mamlaka ya Uhifadhi wa Mji Mkongwe, limekuwa likiathiri utekelezaji wa majukumu ya Idara ya Makumbusho na Mambo ya Kale.

(a) Je, Wizara imechukua juhudi gani kuhakikisha changamoto ya muingiliano wa majukumu ya Idara hizi mbili muhimu inatatuliwa.

(b) Je, kuna athari gani inayojitokeza kutokana na kuwepo kwa muingiliano huo.

<u>Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto:</u>

50. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto:

Kujitolea ni moja ya sifa kuu za wazee na wastaafu wa Zanzibar, ukiachilia mbali kazi ya kuuhifadhi utamaduni wa nchi yetu. Hata hivyo, wazee wetu hawa wamepigania kwa hali na mali kuijenga na kuijengea heshima Zanzibar, na inasikitisha kwamba hadi leo bado wamekuwa ni watu wanaoonekana kutothaminiwa ipasavyo kwa mchango wao mkubwa walioutoa katika nchi hii. Pia kumekosekana mipango thabiti ya kuona matunda ya walichokichuma katika huduma za afya, siha na hata pensheni toshelezi.

(a) Je, Serikali ina mpango gani bora wa kuwashughulikia na kuwapatia mahitaji yao muhimu ili kuwapunguzia uzito wa maisha.

(b) Je, Serikali haioni haja ya kuwa na mpango wa kisheria wa kuwasaidia wazee kupatiwa bima ya afya bure au kwa malipo madogo yanayolingana na pencheni wanayopatiwa sasa.

(c) Je, Serikali haioni haja ya kuwapandishia mafao wazee na wastafu wa Zanzibar ili yawiane na ongezeko la mishahara kwa wafanyakazi wa Serikali.

**<u>Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:</u>**

8. MHESHIMIWA HASSAN HAMAD OMAR (Jimbo la Kojani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Kwa muda mrefu sasa, Serikali ilipiga marufuku usafiri wa meli wakati wa usiku na kwa kuwa siku ya tarehe 27/09/2022, Meli ya AZAM SEA LINK iliondoka kisiwani Pemba saa 10:00 jioni na kufika kisiwani Unguja saa 6:00 usiku na hatimae kupelekea usumbufu mkubwa kwa abiria waliokuwemo kwenye meli hiyo.

(a) Je, Serikali tayari imeshatoa ruhusa kwa vyombo vya baharini vinavyosafirisha abiria kufanya kazi zake usiku.

(b) Kama bado, Serikali imechukua hatua gani kwa kampuni zinazopingana na zuio hilo.

67. MHESHIMIWA SALMA MUSSA BILAL (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Kutokana na kukosa mashirikiano kwa Wizara zetu ambazo hufanya kazi zinazotegemeana, imekuwa ni tatizo kubwa sana hapa Zanzibar hasa kwa Wizara inayosimamia masuala ya barabara ambayo inapelekea barabara karibu zote zilizojengwa kuvunjwa au kuchimbwa kando kando na kupelekea usumbufu mkubwa kwa wenye vyombo vya moto na wendao kwa miguu.

(a) Je, ni kitu gani kinachopelekea kukosekana kwa mashirikiano ya awali ya kuwezesha kuwekwa kabisa kwa miundombinu ya maji kabla ya kujengwa kwa barabara, hali ambayo huchangia kukatwa kwa barabara zetu kwa ujenzi wa barabara hizo.

(b) Kwa nini Serikali inashindwa kuingilia kati suala la kurudi kwa uasili wa barabara zinazovunjwa baada ya matengenezo hayo.

(c) Ni hatua gani Serikali inachukua kukabiliana na urudishaji wa barabara hizi kiasili.

120. MHESHIMIWA SULEIMAN HAROUB SULEIMAN (Jimbo la Kiembesamaki) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Wananchi wa Jimbo la Kiembesamaki wanaipongeza Serikali kwa juhudi inazozichukua katika ujenzi wa miundombinu ya barabara tofauti, ingawaje bado kuna changamoto katika barabara za ndani kwa wananchi wa jimbo hilo ikiwa ni pamoja na shehia ya Mbweni, Shakani na Michungwani hasa inapofikia kipindi cha mvua. Hali hiyo inaathiri baadhi ya shughuli za kiuchumi na kijamii.

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuzitatua changamoto hizo ili kuepusha kadhia kwa wananchi wa maeneo hayo.

## Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

20. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo,Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

Ndege anuai ni viumbe muhimu katika kukuza utalii wa maumbile ya viumbe hai nchini kwetu.

(a) Je, tuna aina ngapi za jamii ya ndege waliopo Zanzibar.

(b) Je, ni aina ngapi kati ya jamii hizo za ndege wamehama na wameshapotea visiwani mwetu kutokana na mabadiliko ya tabia nchi.

(c) Je, Wizara yako inachukua mikakati gani ya kuwahifadhi hawa ndege tulionao kwa maslahi ya taifa letu.

## Wizara ya Maji, Nishati na Madini:

1. MHESHIMIWA HABIB ALI MUHAMED (Jimbo la Mtambwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji, Nishati na Madini:

Mhe. Waziri pamoja na watendaji wako, tumewashuhudia kupitia vyombo vya habari mkipita majumbani na baadhi ya sehemu za biashara, kuwafuatilia watu wanaoiba umeme kinyume na sheria.

Je, ni watu wangapi ambao wamegundulika wameiba umeme kuanzia mwezi wa Januari mpaka Oktoba 2022.

III. **<u>HOJA ZA KAMATI:</u>**

**Mwenyekiti wa Kamati ya Ustawi wa Jamii:**

Hotuba ya kuwasilisha Ripoti ya Kamati ya Ustawi wa Jamii ya mwaka 2022/2023.

Zanzibar, (Raya Issa Msellem)
21 Februari, 2023. KATIBU WA BARAZA.